Nation Media Group
Media of Africa for Africa

www.nationmedia.com
Nation Media Group | Nationmediagroup | @NationMediaGrp

# SHIRIKA LA NATION MEDIA

(Imesajiliwa Kenya chini ya Sheria ya Makampuni)
(Nambari ya Usajili 85/74)

# TAARIFA KUHUSU MKUTANO MKUU WA KILA MWAKA

Taarifa imetolewa hapa kwamba Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Sitini wa Wenyehisa wa Shirika la Nation Media Group PLC utafanyika mtandaoni **siku ya Ijumaa, tarehe 30 Juni 2023 saa 9.00 jioni Saa za Afrika Mashariki** ili kuendesha shughuli zilizotajwa hapo chini.

*Maamuzi yote yataendeshwa kupitia Kura ya maoni.*

**SHUGHULI YA KAWAIDA**

1. Kupokea taarifa za hesabu zilizokaguliwa za kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2022 pamoja na ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakaguzi.

2. Kupokea, kuzingatia na kuidhinisha Ripoti ya Ada ya Wakurugenzi na Ada zilizolipwa kwa Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2022 pamoja na kuidhinisha Bodi kuamua ada za Wakurugenzi Wasio Watendaji.

3. Kuidhinisha gawio pekee la Shs 1.50 kwa kila hisa wa jumla ya kiasi cha Shs 285,442,745 kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2022 kama ilivyopendekezwa na Wakurugenzi. Gawio litalipwa kwa Wenyehisa walio kwenye Sajili ya Wanachama wa Kampuni kufikia mwisho wa siku ya Ijumaa, tarehe 16 Juni 2023 na litalipwa mnamo Ijumaa, tarehe 28 Julai 2023.

4. Kuthibitishia kwamba Wakaguzi wa Hesabu za Kampuni, kampuni ya PricewaterhouseCoopers LLP, baada ya kuonyesha nia yake, itaendelea kuhudumu kama Mkaguzi wa Hesabu za Kampuni kwa mwaka wa fedha wa kampuni unaofuatia kwa mujibu wa kifungu cha 721(2) cha Sheria ya Kampuni ya Kenya 2015 na kuidhinisha Wakurugenzi kuamua ada ya Wakaguzi.

5. Kuchagua tena Wakurugenzi wasio watendaji:
   a) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Dennis Aluanga, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   b) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Louis Otieno, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   c) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Al-Noor Ramji, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   d) kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Stephen Dunbar-Johnson, anastaafu kwa zamu na kwa kuwa anastahiki, amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   e) Dkt. Wilfred Kiboro, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   f) Prof. Lee Huebner, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na hajajitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   g) Bw. Francis. O. Okello, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   h) Dkt. Yasmin Jetha, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;
   i) Bw. Wangethi Mwangi, kwa kufikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na amejitosa ulingoni ili kuchaguliwa tena;

6. Kuteua wanachama wa Kamati ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu ya Kampuni:

   Kwa mujibu wa Kifungu cha 769(1) cha Sheria ya Kampuni ya 2015, Wakurugenzi wafuatao kwa kuwa wanachama wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu wachaguliwe tena ili kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati iliyotajwa:
   a) Bw. Leonard Mususa
   b) Bw. Al-Noor Ramji
   c) Prof. Samuel Sejjaaka

**SHUGHULI MAALUM**

**Kama shughuli maalum, kuzingatia na, ikiidhinishwa, kupitisha maamuzi yafuatayo:**

7. Kama uamuzi wa kawaida

   **"KWAMBA**, kwa mujibu wa Kifungu cha 458 ya Sheria ya Kampuni ya 2015, Kampuni ipewe idhini na hivyo imeidhinishwa kufanya ununuzi wa hisa za kawaida zilizolipiwa na zilizotolewa (zilizorekebishwa kwa hisa za hazina ya kifedha) za Shs 2.50 kwa kila hisa kwenye mtaji wa Kampuni ("**Hisa za Kawaida**") kuhusiana na kampuni kununua hisa zake yaani Hisa za Kawaida kulingana na sheria na masharti yaliyobainishwa kwenye Taarifa ya tarehe 6 Juni 2023 ("**Kampuni kununua hisa zake**") na taarifa hiyo ilitolewa pamoja na taarifa ya mkutano mkuu wa kila mwaka (na inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni), ilisema kwamba:
   a) idadi ya juu zaidi ya Hisa za Kawaida zinazoweza kununuliwa kwa mujibu wa sheria za azimio hili ni Hisa 19,029,516 za Kawaida;
   b) bei ya juu zaidi inayoweza kulipwa kwa ajili ya Hisa ya Kawaida itakuwa Shs 20.00 kama inavyopendekezwa na Bodi;
   c) bei ya chini zaidi inayoweza kulipwa kwa ajili ya Hisa yoyote ya Kawaida itakuwa Shs 2.50 hii ikiwa ni thamani ya sarafu ya hisa hizo;
   d) muda wa mamlaka hii utaisha mwishoni wa miezi 18 kuanzia tarehe ambapo mkutano mkuu wa mwaka wa Kampuni utakaofanyika tarehe 30 Juni 2023, isipokuwa kama ilibadilishwa, kubatilishwa au kufanywa upya awali kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Kampuni 2015; na
   e) Kampuni ina haki ya kuweka akiba ya hisa kama hizo zinazonunuliwa kupitia mpango wa Kampuni Kununua Hisa Zake katika hazina yake."

8. Kama uamuzi wa kawaida

   **"KWAMBA**, kwa mujibu wa Kifungu cha 329 cha Sheria za Kampuni 2015, wakurugenzi wa Kampuni kwa ujumla na bila masharti yoyote, waruhusiwe kugawa upya Hisa za Kawaida ambazo huenda zimenunuliwa na Kampuni kwa mujibu wa kanuni hiyo ya Kampuni kununua hisa zake alimradi mamlaka hii, isipokuwa iwe imewekwa upya, kubadilishwa au kubatilisha na Kampuni, itaisha muda sio baada ya miaka mitano tangu tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa maazimio haya."

9. Shughuli nyingine yoyote ambayo Taarifa yake halali imetolewa.

**Kwa Agizo la Bodi**

Angela Namwakira
Katibu wa Kampuni

Tarehe 8 Juni 2023

**VIDOKEZO:**

1. Kwa mujibu wa vipengee vya sehemu ya 3 ya Sheria ya Kampuni hiyo, 2015, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Biashara (Marekebisho) (Nambari 2), 2021, Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Sitini (AGM) wa Shirika la Nation Media Group PLC ("Kampuni hiyo") utafanywa mtandaoni siku ya Alhamisi, tarehe 30 Juni, 2023 saa 9.00 jioni.

2. Wenyehisa ambao wangependa kushiriki katika mkutano wanapaswa kujisajili kwa ajili ya mkutano wa AGM mtandaoni kupitia https://digital.candrgroup.co.ke au kupitia USSD kwa kubonyeza nambari *483*508# au kupitia kiungo cha Mfumo wa AGM ambacho watatumiwa kwa SMS na/au Barua pepe na kufuata maelekezo mbalimbali kuhusiana na mchakato wa kujisajili. Ili kukamilisha mchakato wa kujisajili, wenyehisa watahitaji kuwa tayari na Nambari zao za Vitambulisho/Pasipoti zilizotumiwa kununua hisa zao na nambari za Akaunti zao za CDSC.

3. Shughuli ya kujisajili kwa AGM itaanza tarehe 12 Juni 2023 saa 03:00 asubuhi na itafungwa tarehe 29 Juni 2023 saa 6 adhuhuri.

4. Ili kupata usaidizi, wenyehisa wanapaswa kupiga nambari zifuatazo za usaidizi: +254 20 8690360 kuanzia 2:00 asubuhi. hadi 10:00 jioni. wakati ujisajili unaendelea. Wenyehisa wowote walio nje ya Kenya wanapaswa kupiga nambari ya usaidizi ili wasaidiwe kujisajili au watume barua pepe kwa digital@candrgroup.co.ke.

5. Kwa mujibu wa Sehemu ya 283 (2) (c) ya Shria ya Kampuni, hati zifuatazo zinaweza kutazamwa kwenye tovuti ya Kampuni kupitia https://www.nationmedia.com
   a) nakala ya Taarifa hii na Fomu ya Mshirika;
   b) Taarifa za Kifedha Zilizokaguliwa za Kampuni za mwaka uliokamilika tarehe 31 Disemba 2022;

6. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali yoyote kwa ajili ya AGM wanaweza kufanya hivyo kwa:
   a) Kutumia kiungo kilichotolewa kupitia sms/baruapepe baada ya kuthibitisha usajili; au
   b) Kufikia AGM Inayofanyika Mtandaoni kupitia https://digital.candrgroup.co.ke au kupitia kiungo cha mfumo wa AGM; Chagua Hudhuria Tukio; Chagua "Nation Media Group Plc AGM"; Chagua kichupo cha chaguo cha "Q&A" na uwasilishe maswali kwenye kisanduku cha matini; au
   c) Kufikia AGM Inayofanyika Mtandaoni kupitia mfumo wa USSD *483*508#; Tumia vidokezo vya menyu ili Uchague chaguo la "Q&A" na watume maswali yao (kwa herufi zisizozidi 160 za matini ya sms); au
   d) Kutuma maswali yao yaliyoandikwa kupitia baruapepe kwenda digital@candrgroup.co.ke; au
   e) Kadiri inavyowezekana, kuwasilisha maswali yao yaliyaondikwa wao wenyewe mahali halisi pa kutuma au anwani ya barua pepe kwa ofisi ya Custody and Registrars Services Ltd, Wasajili wa Kampuni, katika Jumba la IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1, Barabara ya 5th Ngong. Wenyehisa wanaotuma maswali kupitia baruapepe au kuwasilisha kwa C&R Group ni sharti watoe maelezo yao kikamilifu (majina kamili, Nambari ya Akaunti ya Hisa//Nambari ya Akaunti ya CDSC) wanapotuma maswali na ufafanuzi wao. Pia ambatanisha nakala ya Kitambulisho/Pasipoti yako.

   **Maswali kupitia kituo cha AGM**
   Wenyehisa wataweza kuuliza maswali kwenye mfumo wa mtandaoni wa AGM hadi na wakati wa AGM wakitumia kituo cha mtandaoni au msimbo wa USSD.

   **Maswali Mubashara wakati wa AGM**
   Fursa itatolewa kwa wenyehisa kujiunga kwenye AGM mtandaoni ili kuuliza maswali yao wakati wa mkutano. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali yao mubashara wakati AGM ikiendelea wanaweza kujiunga chumba cha mkutano mtandaoni wakati wa AGM (kwa kuchagua kichupo cha "Jiunge kwenye Chumba cha Mkutano wa AGM" katika sehemu ya chini ya dirisha linaloonyesha mtiririko mubashara). Katika chumba cha mkutano, wenyehisa wanaweza kuendelea kutazama tangazo la AGM na ama i) kuchagua chaguo la "inua mkono" kwenye skrini yao ili kuomba fursa ya kuuliza maswali yao moja kwa moja kwa Bodi au ii) kuweka maswali yao kwenye gumzo mubashara ili yasomwe kwa sauti kwa Bodi wakati wa AGM.

7. Wenyehisa ambao wangependa kupiga kura wanaweza kufanya hivyo kwa:
   a) Kufikia AGM Mtandaoni https://digital.candrgroup.co.ke au kupitia kiungo cha mfumo; Chagua Hudhuria Mkutano; Chagua "Nation Media Group Plc AGM"; Chagua kichupo cha chaguo cha "Kupiga kura" na upige kura; au
   b) Kufikia AGM Mtandaoni kupitia mfumo wa USSD kwa kubofya *483*508#; Tumia vidokezo kwenye menyu Kuchagua chaguo la "Kupiga kura" na kufuata vidokezo kadhaa kuhusiana na mchakato wa kupiga kura.

8. Kwa mujibu wa Sehemu ya 298(1) ya Sheria ya Kampuni, wenyehisa walio na haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika AGM wana haki ya kuteua mshirika kupiga kura kwa niaba yao. Si lazima mshirika awe mwanachama wa Kampuni lakini asipokuwa Mwenyekiti wa AGM. Fomu ya mshirika inapatikana kwenye wavuti wa Kampuni https://www.nationmedia.com. Nakala halisi za fomu ya mshirika pia zinapatikana mahali yafuatayo:

   **Ofisi za Custody & Registrars Services Ltd**
   **IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1,**
   **Barabara ya 5th Ngong.**

   Ili iwe sahihi, fomu ya mshirika lazima ijazwe na mwenyehisa au wakili wake ambaye amehalalishwa kupitia maandishi. Ikiwa mwenyehisa ni shirika, chombo kinachoteua mshirika kitatolewa chini ya muhuri ya kawaida (ikiwa ipo) au chini ya mkono wa afisa au wakili aliyehalalishwa wa shirika kama hilo.

   Fomu ya mshirika iliyojazwa inapaswa kutumwa kupitia baruapepe kwa proxy@candrgroup.co.ke katika muundo wa pdf na kuwasilishwa kwa Custody and Registrars Services, IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1, Barabara ya 5th Ngong Nairobi au itumwe kupitia barua posta kwa Custody and Registrars Services, S.L.P 8484-00100 Nairobi ili ifikie kwa Msajili au Katibu wa Kampuni ifikapo saa 9.00 jioni, tarehe 28th Juni 2023.

   Fomu zilizojazwa lazima ziambatanishwe na nakala ya Kitambulisho/Pasipoti halali ya mwanachama na kujumuisha Kitambulisho/Pasipoti, baruapepe au nambari ya simu ya mshirika huyo ili kuwezesha mchakato wa usajili. Mawasiliano kuhusu usajili wowote wa mshirika utakaokataliwa yatatolewa kwa mwenyehisa husika mwisho tarehe 29 Juni, 2023 saa 9.00 jioni ili kuruhusu muda wa kutatua masuala.

9. Mkutano wa AGM utaririshwa moja kwa moja kwa wenyehisa wote ambao watakuwa wamejisajili kushiriki katika mkutano.

10. Wenyehisa waliosajiliwa na washirika wao watapokea ujumbe wa SMS/ na/au baruapepe saa mbili kabla ya AGM, ikiwakumbusha wenyehisa waliosajiliwa na washiria wao kwamba AGM itaanza baada ya saa Mbili na kutoa kiungo cha kutiririsha moja kwa moja.

11. Wenyehisa na washirika waliosajiliwa wanaweza kupiga kura (Mwenyekiti akiwaomba kufanya hivyo) kupitia USSD *483*508# au kwenye Mfumo wa AGM.

12. Kura ya maoni itapigwa kwa maamuzi yote yatakayowasilishwa kwenye taarifa.

13. Matokeo ya AGM yatachapishwa kwenye wavuti wa kampuni (www.nationmedia.com) ndani ya saa 24 baada ya kutamatika kwa AGM.

    Kwa migao ya hisa ambayo haijadaiwa, mbinu inayopendekezwa ya kulipa migao ya hisa ambayo ni chini ya Kshs 150,000 ni kupitia M-PESA. Wenyehisa ambao wangependa kupokea mgao wao kupitia M-PESA na hawajisajili katika njia hii ya malipo wanaweza kuchagua kupokea migao ya siku zijazo kwa kubonyeza *483*038# au kuwasiliana na Share Registrar, Custody & Registrars Services Limited.

    Wenyehisa wote wa sasa na wa zamani wa Kampuni wanaarifiwa hapa kwamba kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Mali za Kifedha ambazo Hazijadaiwa No 40 ya 2011 Sehemu ya II na III, migao na hisa ambazo hazijadaiwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) au zaidi zitahitaji kuwasilishwa kwa Mamlaka Inayoshughulikia Mali ya Kifedha ambayo Haijadaiwa ('Mamlaka hiyo') kama mali iliyotelekezwa katika tarehe iliyoteuliwa.

    Kwa hivyo, wenyehisa wote wa sasa na wa zamani ambao wana migao ambayo hajalipwa wanahitajika kuwasiliana na Share Registrar, Custody & Registrars Services Limited kupitia anwani iliyoashiriwa hapo chini ili kudai migao yoyote ambayo haijalipwa ili kuepuka hatari ya migao kutwaliwa na Mamlaka.

**Custody & Registrars Services Ltd (C&R Group)**
**IKM Place, Tower B, Ghorofa ya 1**
**Barabara ya 5th Ngong, Nairobi**
**Simu + 254 20 760 8216**

OUR BRANDS
NATION Empower Africa. → nation.africa | dembe fm | DAILY NATION | ntv | The EastAfrican | Business Daily | MWANA SPOTI | THE CITIZEN | NTV | TAIFA LEO | TAG brand studio | NATION COURIER SERVICE
NatioNSema | ENNYANDA | NATION FM | NATION ePaper | Daily Monitor | MWANANCHI | KFM | KENYABUZZ | SWAHILIHUB | Spark | NAIROBINEWS